

KULE KUFUNGULIWA KWA MIHURI SABA

Ufunuo 6:1 – 17 “Kisha nikaona hapo Mwanakondoo alipofungua moja ya zile mihuri”

Sikiliza kile Nabii wa Mungu alichosema juu ya hilo:

Tangu kufunguliwa kwa ile mihuri saba, ya wale Malaika nyuma ya mlima kule, Hiki kimekuwa ni kitabu kipya. Ni vile vitu ambavyo vilifichwa vinafunuliwa kama Mungu alivyoahidi katika ufunuo 10 kwamba angefanya. Sisi ni watu tuliopata upendeleo ambao Mungu aliwachagua duniani, kwamba tungeona na kuelewa mambo haya; ambayo siyo hadithi, akili za kimwili za mtu fulani akijaribu kuyatengeneza. Ni Neno la Mungu likidhihirishwa, likithibitishwa kwamba ni sahihi. Kuthibitishwa, siyo kwa sayansi, bali kwa Mungu kwamba ni kweli.

Mungu, kama nilivyosema kabla katika ujumbe, Mungu hahitaji mtu yeyote atafsiri Neno lake. Yeye ndiye mtafsiri wake. Anasema litatokea na linatokea. Analithibitisha hilo; na hiyo ndiyo tafsiri [1]

Kumbuka, ile nguvu ya kuhuisha Angalia yale tunayoona katika siku ya leo. Zile Nguvu za kuhuisha zimekuja kwetu kufungua ile mihuri saba. Ilikuwa ni nini? Akili za mwanadamu? Hapana, Nguvu za kuhuisha za Mungu unaona? Zile nguvu za kuhuisha za Mungu zilizungumza kwamba haya yangetokea, unaona? Kisha Nguvu za kuhuisha za Mungu zikaifanya dunia ishuhudie, kwamba ni kweli. Malaika wa Bwana, kile nilichowaambia kwamba kiko miongoni mwetu, ile Nguzo ya Moto, Nguvu ya kuhuisha, acha dunia ishuhudie kwamba ni kweli. Na katika hilo, hawakujua ni nini, na sisi tuko tunaoangalia upande huu na ni Bwana wetu juu pale unaona?

Yeye ndiye aliyeifungua ile mihuri; Yeye ni ile mihuri kwa maana Neno lote la Mungu ni Kristo, na Kristo ni ile mihuri iliyofunguliwa. Ni nini sasa kule kufunguliwa kwa ile mihuri basi?

Kumfunua Kristo na hasa wale malaika saba waliowakilisha yale makanisa saba walikuwa wote wamekamilika, na hatukuweza hata kuliona hilo. Waliichukua ile picha, siyo sisi. [2] Magazeti yaliionyesha hiyo. Vitabu vinavyotolewa mara kwa mara viliichukua vikaionyesha picha hiyo. Tukaja hapa na kuona siri hizo kuu zilizofichwa kwenye Biblia, zilifunguliwa mbele yetu katika uwanja mpya ambao hatujawahi kuufahamu kabla yake, na yote yanaungana kikamilifu katika kule kuja

kwa Bwana Yesu [3]. Na amesimama pale, akiwa ni Jaji mkuu, akionyesha kwamba Yeye ni Alpha na Omega, Mwanzo na Mwisho. Ni utambulisho wa jinsi gani !.

Nguvu za kuhuisha zimefanya hayo kwetu. Nguvu za kuhuisha zimetufanya tuone kule kuja kwake. Nguvu za kuhuisha zimetunyakua sisi kutoka mautini kuingia uzimani. Nguvu za kunyakua zimetupa upambanuzi wa kujua kile ambacho ni shida yako, na kile unachopaswa kutenda, kile ulichotenda, na kile ambacho ulitakiwa usikifanye, na kile ambacho kingepasa ufanye, na kile utakachokuwa. Nguvu ya kuhuisha mambo hayo yote [2].

Sasa, Mungu alikuwa na makusudi na alikuwa na siri iliyofichwa, na hiyo ndiyo ninayotaka kuzungumza kwa kanisa. Ile siri ya Mungu iliyofichika ambayo alikuwa nayo katika akili zake kabla ya dunia haijaanza na jinsi ambavyo imekuwa ikijiweka wazi yenyewe mpaka sasa hivi katika saa ambayo tunaishi. Unaona? Ndipo utaelewa vizuri kuanzia hapo na kuendelea, ninaamini, kile ambacho kimetendeka.

Ile siri kuu ya Mungu jinsi Ni siri. Aliiweka kuwa siri. Hakuna hata mmoja aliyejua chochote juu ya hiyo; hata malaika hawakujua hilo. Unaona? Hakuifunua hiyo, Hiyo ndiyo sababu katika siri yetu ya saba, wakati muhuri wa saba ulipofunguliwa, kulikuwa na kimya (Ufunuo 8:1).

Yesu, alipokuwa duniani, walitaka kujua ni lini atakuja Naye akasema, “Siyo hata Mwana mwenyewe hajui litatokea lini” (Marko 13: 32-33). Unaona Mungu aliliweka hili kwa ajili yake mwenyewe ni siri. Na ndiyo maana kulikuwa na kimya mbinguni kwa muda wa nusu saa. Na ngurumo saba zikatoa sauti zao, na Yohana alikatazwa kuziandika hizo, kule kuja kwa Bwana (Ufunuo 10:1-7).

Hilo ndilo jambo ambalo bado hajalifunua, jinsi atakayokuja, na ni lini atakuja. NI jambo zuri kwamba haelezei. Hapana. Amelionyesha na kulifunua kwa mifano mingi ambayo iko kwenye Biblia.

Kwa hiyo, Biblia yote ni ufunuo wa siri ya Mungu iliyondani ya Kristo Biblia yote ni udhihirisho wa lengo moja Mungu alilokuwa nalo, Lengo moja alilotaka kulitimiza katika Biblia yote, na matendo yote ya waaminio katika Biblia ilikuwa ni mfano na udhihirisho wa lengo kuu la Mungu lilivyo. Na sasa katika siku hizi za mwisho amelifunua hilo na kulionyesha. Na kwa msaada wa Mungu, tutaweza kuliona asubuhi hii, kile Mungu alichokuwa nacho katika akili yake na amependa kukidhihirisha. Kwa hiyo, ungeweza kuona hiyo maana kuu ya kujua hilo jambo na kujaribu kulileta hilo kwa watu. [4]

Sasa, nyuma kule pale Mwanzoni pa mihuri saba, wakati hawa malaika saba walishuka chini katika umbile la piramidi, wakasimama pale na kuniambia nirudi huku na nizungumze juu ya mihuri hii saba. Naye atakuwa pamoja nami. Alinionyesha mimi hiyo ilikuwa ni nini, vitu vilivyopotezwa. Mimi siku zote niliwaza kuwa imefungwa nyuma ya kitabu na kwamba itakuwa ni kitu fulani ambacho hakikuandikwa katika kitabu; Ila nilielekezwa kwamba hawezi akafanya

hivyo siyo kitu ambacho hakikuandikwa katika kitabu, Ni kitu ambacho kilikuwa kimefichwa katika kitabu. “Kwa maana yeyote atakayeondoa Neno lolote kutoka hilo au kuongeza kwa hilo...” kwa hiyo ni siri ambayo ilikuwa kitabuni katika nyakati hizi saba za kanisa. Kila moja ya hizo ilizaa siri, yote juu ya ubatizo wa maji, na mambo hayo mengine waliyopapasapapasa kwa muda mrefu [5].

Sasa, siri zote za hesabiwa haki kwa imani, utakaso, ubatizo wa Roho Mtakatifu kama ulivyoelewa. Sasa, ni kule kuchukua hizi sehemu zilizoachwa za vile vilivyokuwa vimefichwa kwenye mihuri saba; siyo nyakati saba, mihuri saba ilifunua zile siri. Na halafu akafunua hiki kitu pale juu na akaona mwamba pale, mweupe na haujawahi kuandikwa, hiyo ni siri [6].

Kumbukeni ujumbe wangu hapa? Kule kufunguliwa kwa kile ‘kifuniko’ ambapo zile sauti saba na mihuri haijaandikwa katika Neno la Mungu. Mnakumbuka? Na ikanichukua mimi katika ile piramidi [7].

Mungu alipaswa afungue ile mihuri saba, siyo katika dhehebu. Nimekuwa kinyume nayo siku zote. Bali nje ya madhehebu, ili achukue bibi arusi, siyo bibi arusi wa kidhehebu; Hawezi akafanya hilo. Ni kinyume na Neno lake mwenyewe. Amefungua hizo siri saba pale, na zinaonekana, zinaweka wazi mambo haya yaliyofichwa tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu ... yaweze kufunuliwa siku za mwisho kwa wana wa Mungu. Yakiwa yanaletwa sasa mbele ya watu kwamba wanayaona hayo. Tuko hapo sasa kwa huyu Bibi Arusi asiye kuwa na dhehebu [8].

Muhuri: 1. Ufunuo 6: 1 –2/Matayo Mtakatifu 24: 4 – 5

Kisha nikaona hapo Mwana-kondoo alipofungua moja ya zile muhuri saba, nikasikia mmoja wa wale wenye uhai wanne akisema, kama kwa sauti ya ngurumo, Njoo! Nikaona, na tazama farasi mweupe, na yeye aliyempanda ana uta, akapewa taji, naye akatoka, ali akishinda tena apate kushinda.

Muhuri huu (mfano) una maana ifuatayo:

Mmoja aliyekaa juu yake ni mwigizaji wa Kristo ni mdanganyifu, ana upinde usio na mishale – akimaanisha hana nguvu. Huyu mpandaji katika farasi huyu mweupe alitenda kazi katika hatua tatu kama Mungu katika njia tatu.

Ya kwanza: Alikuwa ni roho ya mpinga Kristo

Ya pili: akawa nabii wa uongo

Tatu: halafu akawa yule mnyama

Unikolai uliitwa upinga Kristo “katika Biblia, kwa sababu ulikuwa kinyume cha mafundisho ya Kristo na ya mitume. Niko ilimaanisha “kushinda” na lai ambayo ina wahuu washirika. Nikolai yamaanisha kuwashinda washirika (Ufunuo 2: 6, 15).

Kwanza ilikuwa ni roho ya mpinga Kristo – halafu ikadhihirishwa kwa namna fulani ya kuzungumza – halafu ikawa fundisho fulani na hiyo ikavalishwa taji katika mtu aitwaye papa. Pale kwenye baraza la Nikea alipewa kiti chake cha enzi. Hii roho ya mpinga Kristo ikakaa ndani ya mtu ambaye aliua kwa roho ya mpinga Kristo uuaji wa kiroho, unikolai. Roma ya kipagani ilibadilika katika muda wetu kuwa Roma ya kipapa (Ufunuo 13). Upako wa Simba ilikuwa ndiyo nguvu ya kushindia kwa wale walioteuliwa (Ufunuo 4: 6 – 7).

Muhuri:2. Ufunuo 6: 3 – 4/Mt. Matayo 24:6

Na alipoifungua muhuri ya pili, nikamsikia yule mwenye uhai wa pili akisema, njoo! Akatoka farasi mwingine, mwekundu sana, na yeye aliyempanda alipewa kuindoa amani katika nchi, ili watu wauane, naye akapewa upanga mkubwa.

Farasi mwekundu anawakilisha utawala. Naye anayemuendesha ni Nabii wa uongo – papa – na akapewa mamlaka ya kuondoa amani duniani, kwamba wauane wenyewe. Nguvu ya kidini – wafia dini wengi (68 milioni). Aliua kwa upanga. Nguvu za siasa, kanisa na taifa viliungana. Kile kilichoonekana ni kitu kisicho kibaya ushawishi wa roho ya kidini ukageuka kuwa kichwa cha mtu aliyevikwa taji mwenye kanisa lenye kiu ya damu. Kila mpinzani alionewa na kuuwawa. Lakini upako wa ng’ombe uliokuwa juu ya washindi ulipingana na hiyo roho.

Muhuri: 3. Ufunuo 6:5 – 6/Mt. Matayo 24: 7 – 8

Na alipoifungua Muhuri ya tatu, nikamsikia yule wa tatu mwenye uhai akisema, Njoo! Nikaona na tazama, farasi mweusi na yeye aliyempanda ana mizani mkononi mwake. Nikasikia kama sauti katikati ya hao wenye uhai wanne, ikisema kibaba cha ngano kwa nusu rupia, na vibaba vitatu vya shayiri kwa nusu rupia, wala usiyadhuru mafuta wala divai.

Farasi mweusi na aliyekaa juu yake alikuwa na mizani mkononi mwake. Sasa, aliua mafundisho yake. Alifanya hivyo kupitia mvinyo ya uasherati wake, alipima chakula na kuhesabu gharama yake. Barua za vitubio ziliuzwa, vibali vya kutenda dhambi zilizolipiwa, fundisho la kitubioni. Papa amejipasisha mwenyewe kama “mwakilishi wa mbinguni na duniani na kitubioni”. Taifa na kanisa vimeungana. Kanisa lilitaka fedha kwa maombi ya vibali vilivyotolewa kwa dhambi ambazo bado kutendwa. Waamini walinyonywa.

Lakini upako wa mwanadamu ulikuwa juu ya wale waliokuwa washindi.

Muhuri: 4. Ufunuo 6: 7 – 8/Mt. Matayo 24: 7 - 8

“Na alipoifungua Muhuri ya nne, nikasikia sauti ya yule mwenye uhai wa nne akisema, Njoo! Nikaona, na tazama, farasi wa rangi ya kijivu juu, na yeye aliyempanda jinalake ni Mauti, na kuzimu akafuatana naye. Nao wakapewa mamlaka juu ya robo ya nchi, waue kwa upanga kwa njaa na kwa tauni na kwa hayawani wa nchi”.

Farasi wa kijivujivu. Na yule aliyempanda anaitwa mauti” kuzimu (jehanamu) akafuatana naye. Na akapewa mamlaka juu ya robo ya watu duniani, kuwauwa kwa upanga, na njaa na mauti Huu ni wakati wa sasa wa Laodikia (Ufunua 3:14 – 21) Kutokana na rangi nyeupe, nyekundu na nyeusi Nguvu hizo zimechanganyika kuleta farasi wa rangi ya kijivujivu. Ya kidini, nguvu za kisiasa na mapepo vimechanganyikana = mauti (kutengwa na Mungu). Kifo cha kiroho hutokea kwa kuchanganya. Kwa hiyo jina la huyo anayempanda farasi wa kijivujivu anaitwa: mauti Ufalme wa shetani unaanza kudhihirika juu ya nchi. (Edeni ya shetani inafikia kumalizika/mwisho katika siku 6 = miaka 6,000). Mpinga Kristo anaendeshwa katika maangamizi na kuzimu kunamfuata Yeye.

Lakini upako wa tai unaishinda hii roho (Ufunuo 4:6-7)

Muhuri: 5. Ufunuo 6:9-10/Mt. Matayo 24:9-11

Na alipoifungua muhuri ya tano, nikaona chini ya madhabahu roho zao waliochinjwa kwa ajili ya Neno la Mungu, na kwa ajili ya ushuhuda waliokuwa nao, wakalia kwa sauti kuu, wakisema Ee Mola, Mtakatifu, mwenye kweli, hata lini kutohukumu, wala kuipatia haki damu yetu kwa hao wakaa juu ya nchi?

Roho za waliochini ya madhabahu ni wayahudi waliochaguliwa kimbele ambao wameuawa katika nyakati zote. Wayahudi halisi wa kweli, walioishi maisha ya utauwa/kimungu waliishi chini ya dini ya kiyahudi – walia kwa ajili ya kulipiwa kisasi, kama katika agano la kale.

Muhuri huu unaonyesha pia kwamba roho za waliokufa haziko usingizini/hazikulala (Ni miili tu ya kidunia ndiyo ambayo imelala makaburini).

Muhuri: 6. Ufunuo 6:12 – 17/Mt. Matayo 24:29 – 31/Isaya 13:6-11

Nami nikaona, alipoifungua muhuri ya sita, palikuwa na tetemeko kuu la nchi, jua likawa jeusi kama gunia la singa, mwezi wote ukawa kama damu, na nyota zikaanguka juu ya nchi kama vile mtini upukutishavyo mapooza yake, utikiswapo na upepo mwingi. Mbingu zikaondolewa kama ukurasa ulivyokunjwa, na kila mlima na kisiwa kikahamishwa kutoka mahali pake. Na wafalme wa dunia, na wakuu, na majemadari, na matajiri, na wenye nguvu, na kila mtumwa, na muungwana, wakajificha katika pango na chini ya miamba ya milima, wakiiambia milima na miamba, tuangukieni, tusitirini, mbele za uso wake Yeye aketiye juu ya kiti cha enzi na hasira ya mwanakondoo. Kwa maana siku iliyo kuu ya hasira yake, imekuja naye ni nani awezaye kusimama? Siku kuu ya hasira. Muhuri huu (alama) una maana zifuatazo Dhiki Kuu. Dhiki za maumbile kwa Wayahudi na kwa kanisa siyo Bibi arusi), na kwa walio waovu duniani [16].

Sasa, tunaona pia kwamba muhuri wa sita sasa ukiwa umefunguliwa. Ilikuwa ni kwa makusudi matatu. Sasa, makusudi yenyewe ni haya: Jambo la kwanza ni hili mwanamwali mpumbavu inabidi aingie kwenye dhiki kuu kwa ajili ya kutakaswa.

Inabidi atakaswe kwa dhambi zake za kutokuamini na kukataa ujumbe. Haya yanafanyika wakati wa dhiki kuu.

Sasa, yeye sio Bibi Arusi, ila ni kanisa, watu wasafi ambao hawakupata nafasi, pengine, kupokea ujumbe, au kwa njia nyingine walipofushwa na hawa manabii wa uongo, na hawakupata nafasi, na bado walikuwa wanyoofu katika mioyo yao, na Mungu anajua mioyo yao, na wako hapa wanatakaswa wakati huu (Ufunuo 7: 9-17).

Angalia sasa kule kutakaswa kwingine; huku ni kwa Waisraeli wanapokusanyika. Hilo ni kusudi la pili. Mungu anawatakaswa Waisrael wakati wa dhiki kuu. Kati ya mamilioni watakaokusanyika pale, kutakuwa na waliochaguliwa mia moja arobaini na nne elfu. (Ufunuo 7:1-8), na watatakaswa pia. Mungu atawatakaswa waisraeli.

Angalia, dunia nzima itakuwa inatakaswa. Litakuwepo jambo ambalo mwezi, nyota, na maumbile yote yatatakaswa. Unaona itakuwa ni nini? Dunia itajifanya upya yenyewe, ikitakaswa, inakuwa tayari kwa utawala wa miaka elfu. Ule utawala wa miaka elfu unakuja. Na angalia kila kitu kilicho na uchafu ndani yake kitakuwa kinatakaswa katika muhuri wa sita [9].

Tuko katika utungu – Kristo, kumtoa Bibi arusi. Kila kitu kinaugua katika utungu wa uzazi. Unaona, jambo fulani liko karibu kutokea. Na pigo la sita linaiacha iingie utakasoni! Ndugu, dunia itatetemeka kujifungua yenyewe, nyota zitatikiswa, volkano itapasuka na dunia itajifanya upya. Lava mpya ya volkano itatoka katikati ya dunia na kufunika kila kitu [17].

Chini ya muhuri huu wa sita, wale mapepo 200,000 wa kimiujiza (wakidini) mapepo ya kimiujiza walifunguliwa kwa wayahudi kupitia Stalin, Hitler, mtesaji wa wayahudi, na ilianza Roma, Ujerumani (Ufunuo 9:13 – 21).

Muhuri: 7. Ufunuo 8: 1-5/ufunuo 10/Mt. Matayo 24:32

“Hata alipoifungua muhuri ya saba, kukawa na kimya mbinguni kama muda wa nusu saa. Nami nikaona wale malaika saba wasimamao mbele za Mungu, nao wakapewa baragumu saba. Na malaika mwingine akaja akasimama mbele ya madhabahu, mwenye chetezo cha dhahabu, akapewa uvumba mwingi, ili autie pamoja na maombi ya watakatifu wote juu ya madhabahu ya dhahabu, iliyo mbele ya kiti cha enzi. Na moshi wa ule uvumba ukapanda mbele za Mungu pamoja na maombi ya watakatifu, kutoka mkononi mwa malaika. Na huyo malaika akakitwaa kile chetezo, akakijaza moto wa madhabahu, akautupa juu ya nchi, kukawa radi na sauti na umeme na tetemeko la nchi.”

Sasa, angalia, wakati wa kufunguliwa kwa muhuri wa saba, Ufunuo 10, Neno kamilifu litazaliwa katika udhihirisho tena na kuthibitishwa na Roho wa Mungu katika ukamilifu wa nguvu zake, kama ilivyokuwa wakati lilipokuwa hapa duniani. Amen. Waebrania 13:8 ilisema Yesu Kristo ni yule yule jana, leo na hata milele. Katika Mt. Luka 17:30 Yesu alisema”Katika siku za mwisho, kama ilivyokuwa siku

za Sodoma wakati mwana wa adamu atakavyojifunua mwenyewe tena, itakuwa ni jambo lile lile”

Dunia iko katika hali ya Sodoma na kanisa limeenda Sodoma pamoja na Loti na mke wake. Na ninasema hili kuna kanisa lililochaguliwa mahali fulani katika dunia hii ambalo limejitenga pembeni kutoka kwenye mambo haya. Na udhihirisho wa Mungu umevuta usikivu wake, tuko katika siku za mwisho [10].

Sasa ufunuo sura ya 8 unafunua tu mahali muhuri wa saba unapofunuliwa ambapo hakuna chochote kinachofunuliwa. Sasa, hakuna chochote ambacho hakikufunuliwa katika muhuri wa saba. Sasa, hauhusiani chochote na sura ya 7 ya ufunuo. Ni ufunuo wa muhuri wa saba ambao ni kimya kikamilifu. Na kama tu ningekuwa na muda (nitajaribu sehemu chache) kuwaonyesheni kutoka mwanzo Ambapo huu muhuri ya saba unazungumziwa. Kutoka kule mwanzoni katika kitabu cha Mwanzo, huu wa saba Hii muhuri imesogea kuja juu [11].

Muhuri wa saba, kwa maana kinachofuatia ni siri ya kuja kwa Kristo [12].

Yesu Kristo alipokuwa hapa duniani, nadhani hakuna moja ya tatu ya kabila la wayahudi waliojua kwamba alikuwepo. Wanaweza wakawa wamesikia habari za mzushi chini kule mahali fulani, lakini hawakulitilia maanani hilo, waliendelea tu “Alikuja kwa walio wake na walio wake hawakumpokea”.

Sasa, hapo ndipo ninaamini kuwa sasa, haikusemwa kwamba atakuja kisiri, ingawa unyakuo utakuwa ni siri. Kwa hiyo kama kuja kwake kulikuwa ni siri, itakuwa ni kitu cha siri sana ule unyakuo hautajulikana. Kwa wazi au moja kwa moja watasema, ‘vema nilifikiri tulipaswa kuwa na unyakuo na hukumu hizi zote juu ya uso wa nchi” Atasema umeshakuwepo na hamkujua jambo hilo [13].

Angalieni, nataka kusema jambo moja, kwa karibu sasa. Msilikose hili. Jinsi inavyostaajabisha. Kutoka yule malaika wa saba (ambaye ni mjumbe wa muhuri wa saba) ujumbe (na Ufunuo 10 ulikuwa muhuri wa saba) kule kwenye Tarumbeta saba, katikati ya nyakati hizi oh Mungu, tutalisemaje hili ili kuwafanya watu waelewe? Ni katikati ya Tarumbeta ya sita (na tarumbeta ya sita na muhuri wa sita vyote vinatoa sauti zao wakati mmoja) na katikati ya Tarumbeta ya sita na na tarumbeta ya saba, hapo atatokea Nabii kwa watu wa Mataifa kuwaita watu warudi katika mafundisho yale ya kwanza ya Pentekose; na halafu wale mashahidi wawili wa ufunuo 11 wanatokea kwa wayahudi ili wawapeleke kwa Yesu, wakati kanisa linachukuliwa juu manabii hao wote. Amen. Neno la Mungu haliwezi kuvunjwa. Haitakuwa ni dhehebu. Unalionga hilo? [12]

Sasa, umeona katika kufunguliwa kwa muhuri wa saba, nao pia una siri ya makusudi matatu. Hii moja ninayo, itazungumza na imezungumza, kwamba ni siri ya zile ngurumo saba. Na hizo ngurumo huko mbinguni zitafungua hii siri. Itakuwa wakati hasa wa kuja kwa Kristo, kwa sababu Kristo alisema hakuna ajuaye anarudi lini.

Je uliona vile wayahudi walimuuliza Yeye hilo? Kule kuja kwake, na saa ya kuja kwake, wakati uharibifu/maangamizi ya dunia unajua, alisema pale, “Ishara gani itakuwa ya kule kuja kwa mwisho wa dunia”? katika Matayo 24, ndipo pale walipomuuliza swali hilo. Alilifuatilia hilo. Aliwaambia kuhusu waisraeli watakavyokusanywa kama taifa katika mstari wa 31 matayo 24. Lakini tena alianza kwa mifano unaona? Halafu unaona pale. “Jifunzeni kwa mfano wa mtini. Unapouona unachipua, kwa nini, unajua wakati wa mavuno u karibu” na “halafu muonapo mambo haya (ya kuja) yanatokea mnajua wakati uko karibu”

Unaona Israeli wanakusanyika katika nchi yao ila ukiangalia aliacha ufunuo wa muhuri huu wa saba. Na hapa wakati muhuri ya saba, alipoifungua, aliua cha tena unaona? Sasa tunaona ya kuwa ni siri kamilifu.

Kwa hiyo, saa haijafika bado ya siri hii kujulikana, tuko umbali huu na yaliyobakia yatajulikana hasa wakati unapokaribia kwa Yesu kutokea hapa duniani tena kwa Bibi arusi wake au chochote kile kitakachofanyika wakati huo.

Sasa mpaka wakati huo tuendelee kuomba na kuishi maisha yaliyonyooka ya kikristo tukiangalia mbele juu ya kule kuja kwake.

Unajua tulipolinganisha maandiko Matayo 24 na ile muhuri sita, muhuri wa saba uliachwa nje, kwa sababu, Kristo alisema Mungu peke yake anajua, hata malaika hawajui. Sio ajabu, hata haikuandikwa unaona, walinyamaza; hakuna kilichofanyika, Malaika hawajui hilo; hakuna hata mmoja ajuaye wakati atakapokuja. Kutakuwa na sauti saba za hizi ngurumo ambazo zitafunua ufunuo huu mkuu wakati huo.

Kwa hiyo ninaamini, kama hatulijui hilo, na haitajulikana mpaka wakati huo, lakini litafunuliwa katika siku ile, saa ile inayopaswa kufunuliwa. Kwa hiyo jambo litupasalo sisi kufanya mbele za Mungu ni kwenda kwa unyenyekevu na kumtumikia Yeye, na kufanya yote ambayo tunajua namna ya kuyafanya, na kuishi maisha mazuri ya Kikristo.

Hapa sasa, tunaona kuwa muhuri wa sita umefunguliwa kwetu; tunaona na tunajua kwamba ule muhuri wa saba hauwezi ukavunjwa mbele za watu mpaka saa hiyo ifike.

Sasa, kulikuwa na sababu ya Mungu kuacha hizi sauti saba zingurume, kwa sababu ni lazima zije, kwa maana tunaona kwamba Kristo, Mwanakondoo alikichukua kitabu, mkononi mwake, na akafungua ule muhuri wa saba (Ufunuo 5:1-10). Lakini unaona, ni siri iliyofichwa. Hakuna hata mmoja ajuaye ila iko inakubaliana na alivyosema; hakuna atakayejua kule kuja kwake; Pia wao hawatajua juu ya siri ya ngurumo hizi saba. Kwa hiyo unaona, imeunganishwa pamoja.

Kiasi hicho tunafahamu/tumeelewa leo, kwa sababu sehemu iliyobakia imewekwa wazi, lakini sehemu hii haikuwekwa wazi. Lakini nilipokuwa chumbani kwangu, na

nikaisikia, ila nikaiona ikifunguka kwa hizi ngurumo saba. Sasa, hapo ndipo tu tunapoweza kufikia hatuendelei. Na sasa naamini kwamba kila mmoja wenu atamtumikia Mungu, na Mungu ataangalia yaliyobakia.

Sasa, tuko ndani ya ule mwisho sasa, kwa neema ya Mungu, siri zote za ile mihuri sita ambayo ilikuwa imefungwa na tunaolewa nakujua kwamba muhuri wa saba hautakiwi ueleweke kwa watu wote [9].

Sasa, siri ya kitabu inafunuliwa wakati mihuri inapovunjwa. Na wakati mihuri imevunjwa kabisa, muda wa ukombozi utakuwa umeisha, kwa sababu Mwanakondoo ataondoka kwenye sehemu ya maombezi ili achukue madai ya haki yake. Alikuwa mpatanishi katika hilo, lakini wakati ufunuo halisi wa mihuri unapotokea juu ya mihuri inapoanza kufunguka, Mwanakondoo anaondoka kwenye kiti cha rehema. Hiyo ni sawa na Neno. Tulisoma usiku uliopita. Alitoka katikati na akachukua kile kitabu. Kwa hiyo Yeye siyo mpatanishi tena, kwa sababu hata waliomwita Yeye ni Simba na huyo ni mfalme naye siyo mpatanishi hapo [14].

Sasa, hebu tugeukie Ufunuo 8:1 lazima tukumbuke kwamba Muhuri huu wa saba ni mwisho wa wakati wa mambo yote. Hiyo ni kweli. Mambo yaliyoandikwa katika kitabu cha mihuri saba kimefunga mpango wote wa ukombozi kabla ya kuwekwa misingi ya dunia yote inaisha. Ni mwisho ni mwisho wa dunia ya mahangaiko. Ni mwisho wa mahangaiko ya maumbile. Ni mwisho wa kila kitu. Pale ni mwisho wa tarumbeta. Ni mwisho wa vile vitasa. Ni mwisho wa dunia. Ni mwisho wa wakati. Wakati umeisha; Biblia ilisema hivyo.

Ufunuo sura ya kumi mstari 1 – 7 muda umeisha. Malaika alisema, ”Hakuna wakati tena”, wakati wa siku za tukio hili kuu kutokea. Kila kitu wakati umeisha, mwishoni mwa muhuri wa saba.

Angalia, ni mwisho wa wakati wa kanisa. Ni mwisho wa mihuri saba. Ni mwisho wa tarumbeta. Ni mwisho wa vitasa, na hata inamaliza na kuingia utawala wa miaka elfu; hivyo ni katika muhuri wa saba.

Ni kama kuwasha roketi hewani, nayo inalipuka hapa na inakwenda juu, halafu inalipuka tena, inatoa nyota tano. Nyota inalipuka inaleta nyota tano kutoka kwa moja; inazidi kutoweka. Hivyo ndivyo ulivyo muhuri wa saba; inamaliza muda kwa dunia. Inamaliza muda kwa hiki. Inamaliza muda kwa kile. Inamaliza muda kwa kile. Inamaliza muda Kila kitu kinaisha tu kwenye muhuri wa saba.

Sasa, atalifanyajefanyaje? Hiyo ndiyo hatujui, si ndiyo? Hatujui. Ni wakati hata wa mambo yote, na kuingia katika utawala wa miaka elfu.

Angalia, kuvunjwa kwa muhuri huu ilikuwa ni kitu kikubwa sana kiasi kwamba mbinguni walishangazwa na hilo kwa kimya cha muda wa nusu saa sasa, ni kuu? Ni nini? Walishangazwa. Mbinguni hakuna kilichosogea kwa muda wa nusu saa.

Sasa, Nusu saa inaweza isiwe kubwa kama una wakati mzuri, lakini kama ni mahali pasipoamulika kati ya kifo na uzima, itaonekana kama miaka elfu. Ilikuwa ni kuu sana, Yesu kamwe hakulitaja. Hata wengine waliobaki Yohana hakuweza kuandika juu ya hilo. Hapana, alikatazwa asiandike hapa. Unaona, kuna tu Hakuandika, lakini ni kimya tu [15].

Sasa, mara tu hili kanisa, bibi arusi amekusanywa pamoja, anachukuliwa juu; katika ile siri ya muhuri wa saba; ile siri ya kuondoka. Na wayahudi wanaitwa kwa siri ya tarumbeta saba, ambayo ni manabii wawili, Eliya na Musa. Na wanakuja, na hapo ndipo wapentekoste wanapochanganyikiwa. Wanategemea jambo fulani litokee, na kanisa limekwisha kuondoka, na hiyo ni kwa Wayahudi [12].

Nukuu za Kiingereza:

- [1] Nguvu ya Mungu ya kubadilisha Aya 77 [2] ni kule kuchomoza kwa jua Aya 189 – 191
- [3] Kutaharuki Aya 53/ [4] Kristo ni siri ya Mungu iliyofunuliwa uk. 17
- [5] Chakula cha kiroho kwa wakati wake Aya 83 [6] kule kutoka uk. 42
- [7] Shutuma kwa Neno uk.8 [8] Muungano usioonekana wa Bibi arusi, uk 43
- [9] Muhuri wa saba kitabu cha mihuri uk. 575 – 577 Aya 178 – 181 + 182 – 188
- [10] Ile mbegu haitarithi pamoja na kapi uk. 19; Aya 101 – 102
- [11] Muhuri wa saba uk. 536 Aya 38/ [12] Karamu ya Tarumbeta uk 36 + 39
- [13] Muhuri wa tatu uk. 238, Aya 38 – 39 [14] Muhuri wa kwanza uk 124 – 125 aya 29
- [15] Muhuri wa saba uk 555 – 556 Aya 102 – 107
- [16] Muhuri wa sita uk. 422 [17] Muhuri wa sita uk 439 – 440

Jiwe la kiroho la kujengea na 157 kutoka kwenye Neno lililofunuliwa la saa hii, Yamekusanywa na Gerd Rodewald Friedenstr. 69, D-75328 Schomberg, Germany, Simu (+49) 72357613, Fax (+49) 72353306

Anakuja mmoja na ujumbe ambao ni moja kwa moja ni Biblia na kazi ya haraka itazunguka dunia. Na mbegu zitaingia magazetini, vitu vya kusomea, mpaka kila mbegu iliyochaguliwa kimbele imesikia (Ndugu Branham katika mwenendo utaratibu na mafundisho uk. 724).

Kwa nakala zaidi za kiingereza au kiswahili Andika kwa:

*Charles E.Y. Kanju
Box 5138, Tanga
E-mail: chaelika@Hotmail.com
cellphone: 0784 704299*